# MAJI TANZANIA

TOLEO NA 018

OKTOBA- DESEMBA, 2021




## Rais Samia aipa tano Sekta ya Maji

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ameridhika na maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa maji wenye thamani ya Sh. bilioni 520 unaotekelezwa na Wizara ya Maji kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha (AUWSA) katika Jiji la Arusha na kusisitiza kukamilika kwa wakati.



## Wizara ya Maji yapokea Bilioni 139.4. Miradi ya maji 218 kutekelezwa

## Rais Samia Awapa Majisafi Longido, Awataka kulinda Miundombinu ya Mradi



# Rais Samia aipa tano Sekta ya Maji

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ameridhika na maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa maji wenye thamani ya Sh. bilioni 520 unaotekelezwa na Wizara ya Maji kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha (AUWSA) katika Jiji la Arusha na kusisitiza kukamilika kwa wakati.

Rais Samia amesema mradi huo utamaliza changamoto ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama, pamoja na usafi wa mazingira katika Jiji la Arusha ambalo limekuwa na changamoto ya maji kwa muda mrefu.

Amesema hayo baada ya kukagua moja ya vituo vya kusukuma maji vya mradi huo kilichopo katika eneo la Chekereni katika Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha.
"Mradi umeshaanza kutoa huduma katika baadhi ya maeneo na kufikia mwezi Juni, 2022 wananchi wote wa Arusha watakuwa wakipata majisafi na salama", Rais Samia amesema.

Awali, Waziri wa Maji, Mhe. Juma Aweso (Mb) amesema kwa sasa asilimia 63.45 ya wakazi wa Jiji la Arusha wanapata huduma ya majisafi na salama na wakazi 4,000 wananufaika na huduma ya majitaka. Waziri Aweso amesisitiza kuwa huduma itafika mpaka maeneo ya vijijini kwa kuwa mradi huo ni mkubwa na uzalishaji wake ni lita milioni 200 za majisafi kwa siku wakati mahitaji ya majisafi kwa Jiji la Arusha kwa siku ni lita milioni 109.

Ujenzi wa mradi huu umefikia asilima 75, na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2022. Utaongeza uzalishaji wa majisafi kutoka wastani wa lita 40,000,000 hadi lita 200,000,000 kwa siku na utawezesha utoaji wa huduma ya majisafi kufikia zaidi ya asilimia 100 katika jiji la Arusha.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiongea na wakazi wa Jiji la Arusha kuhusu huduma ya majisafi*





# Wizara ya Maji yapokea Bilioni 139.4. Miradi ya maji 218 kutekelezwa

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan amefungua mradi wa maji wa Longido wenye thamani ya shilingi bilioni 15.7, na kuwataka wananchi kuulinda mradi huo ambao ni mali yao.

Mhe. Samia amefungua mradi huo katika eneo la Stendi Mpya, Longido wakati wa ziara yake ya kikazi ya siku mbili mkoani Arusha, ambapo ameelekeza vyombo husika vichukue hatua kwa yeyote atakaye fanya uharibifu katika miundombinu ya mradi huo ambao chanzo chake kipo mkoani Kilimanjaro.

"Mradi huu utaleta mabadiliko makubwa katika eneo hili, na kuufanya mji kuendelea zaidi, tuhakikishe tunalinda miundombinu yake" Mhe. Samia amesema na kuwapongeza watendaji wa Sekta ya Maji kwa kufikisha huduma ya majisafi kwa wananchi, jambo ambalo ni baraka na sadaka. Aidha, amewataka wananchi kulipa bili za maji ili wataalam wa maji waweze kuhudumia mradi huo ipasavyo.

Awali, Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akiongea katika hafla hiyo, ameshukuru kwa Wizara ya Maji kuongezewa shilingi bilioni 207 katika bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ya kiasi cha shilingi bilioni 600 kwa mwaka 2021/22, ambapo amesema kiasi hicho kitatekeleza idadi ya miradi ya majisafi 1176.



Waziri Aweso, pamoja na hilo ameshukuru kwa kupokea kiasi cha shilingi bilioni 35 ambazo zitatumika kulipa wakandarasi waliojenga miradi ya maji.

Mradi wa maji wa Longido umeanzia mkoani Kilimanjaro na kutekelezwa na Wizara ya Maji kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha (AUWSA). Mradi huo umeondosha changamoto ya upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa matumizi ya binadamu, pamoja na mifugo kwa wakazi wa Longido.




***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akifungua mradi wa majisafi wa Longido wenye thamani ya shilingi bilioni 15.7***





# Rais Samia Awapa Majisafi Longido, Awataka kulinda Miundombinu ya Mradi

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema serikali imetenga jumla ya shilingi Bilioni 139.4 kwa ajili ya Wizara ya Maji ambapo fedha hizo zitaelekezwa katika kutatua changamoto ya huduma ya maji kwa Watanzania.

Akizungumza na waandishi wa habari Mhe. Aweso amesema fedha hizo zimetokana na mkopo wenye masharti nafuu uliotolewa na Benki ya Dunia kupitia Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19 ambapo Tanzania ilipewa kiasi cha Dola za Kimarekani Milioni 567 sawa na takriban shilingi trilioni 1.3.

“Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais shupavu Mhe. Samia Suluhu Hassan inatambua kwamba Maji ni rasilimali muhimu kwa ajili ya uhai wa binadamu, wanyama, mimea, mazingira na uchumi kwa ujumla. Kutokana na hilo, katika fedha hizo, Wizara ya Maji ambayo ndiyo yenye jukumu la kuhakikisha Watanzania wanapata majisafi, salama na yenye kutosheleza karibu na makazi yao imepangiwa jumla ya shilingi bilioni 139.4 sawa na asilimia 10.6 ya fedha hizo.” Waziri Aweso amesema.

Ameainisha matumizi ya fedha hizo kuwa shilingi Bilioni 104 zitatekeleza jumla ya miradi ya maji 218 nchini , ambapo miradi 172 itatekelezwa mijini na miradi 46 itatekelezwa vijijini. Miradi hiyo itawezesha idadi ya wananchi milioni mbili kupata huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza. Shilingi Bilioni 17.5 zitatumika kununua seti 25 za mitambo kwa ajili kuchimba visima ambapo kila mkoa utapata mtambo mmoja.

Shilingi Bilioni 17.6 zitatumika kununua seti tano za mitambo ya ujenzi wa mabwawa na vifaa vya utafiti wa maji chini ya ardhi ili kuondoa changamoto ya upatikanaji wa maji katika maeneo ambayo hakuna vyanzo vya uhakika vya maji.

Amemshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuwajali Watanzania na hasa akina mama ambao huachiwa jukumu la kuhakikisha maji yanakuepo katika makazi kwa huduma mbalimbali za kifamilia.

Waziri Aweso amewataka viongozi wa Wizara ya Maji kuhakikisha wanasimamia matumizi ya fedha hizo vizuri.




*Menejimenti ya Wizara ya Maji, pamoja na viongozi walioshiriki katika kikao kuhusu utekelezaji wa miradi ya maji kupitia fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO.*






*Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akitoa Tuzo kwa maabara za Ubora wa Maji zilizopata Ithibati, ambapo hivi sasa maabara saba za ubora wa maji zimekidhi vigezo vya kimataifa na zinaweza kufanya kazi ya kuangalia ubora wa maji mahali popote Duniani*



# Miradi sita muarobaini wa changamoto ya Maji Mbeya

Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga amezitaka Bodi za Maji za Mabonde nchini kuwa na mikakati mahsusi kwa ajili ya kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi ili kuzuia athari zake ikiwemo athari katika vyanzo vya maji.

Mhandisi Sanga ametoa maelekezo hayo katika hafla fupi ya kusaini makubaliano ya utendaji baina ya Wizara ya Maji na Bodi za Maji za Mabonde kwa mwaka 2021/22 katika Ukumbi wa Mikutano wa Wizara ya Maji, Mji wa Serikali jijijni Dodoma.
Lengo la makubaliano hayo ni kuongeza ufanisi wa mabonde tisa ya maji yaliyopo nchini.

"Tumeona athari za mabadiliko ya tabianchi zilivyoathiri maeneo mbalimbali nchini mwaka huu hadi kusababisha upungufu wa maji kwenye vyanzo vingi vya maji. Ili kuepuka hali ya aina hii isijirudie, Bodi zote za Mabonde zifanye tathmini ya kina kuhusu changamoto zilizotokea na kuweka mikakati mahsusi ili kukabiliana na athari zote zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi. Tuhakikishe mvua zinazonyesha zinakuwa na manufaa kwa kujenga mabwawa kwa ajili ya kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadaye na hasa katika kipindi cha ukame," Mhandisi Sanga ameelekeza kwa watendaji wote wa Sekta ya Maji katika mabonde.

Pia, Mhandisi Sanga amezipongeza bodi hizo kwa kuongeza kiwango cha ufanisi kutoka asilimia 51 mwaka 2019/2020 hadi kufika asilimia 75.2 kwa mwaka 2020/2021 na kuzitaka kuongeza msukumo katika ukaguzi wa vibali vya maji vinavyotolewa kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya maji kwa wateja wote mara kwa mara kwa lengo la kuhakikisha matumizi yake yanaendana na kibali kilichotolewa kisheria wakati wote kwa lengo la kupunguza matumizi yasiyo sahihi yanayoleta changamoto kwenye vyanzo vingi vya maji.

Awali, akiongea katika hafla hiyo Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Nadhifa Kemikimba amewataka Maafisa Maji wote wa Bodi za Maji za Mabonde kuwa mabalozi wazuri kwa kuwasaidia viongozi wa Wizara na Serikali kwa ujumla kusimamia vizuri na kutatua changamoto zote kwenye mabonde ya maji kwa kuwa maji ni hitaji la msingi kwa maendeleo ya taifa.

Aidha, Mwenyekiti wa Maafisa Maji wa Bodi za Maji za Mabonde nchini, ambaye pia ni Afisa Maji wa Bodi ya Maji ya Bonde la Pangani, Bw. Segule Segule amesema watahakikisha wanatimiza malengo yote waliyowekewa kwa ufanisi ili rasilimali za maji ziwe chachu ya maendeleo ya taifa.




*Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Anthony Sanga akikabidhi mkataba wa utendaji kazi kwa mmoja wa Maafisa Maji wa Mabonde katika ofisi za wizara, mji wa Serikali Mtumba*



# Miaka 60 ya Uhuru, na Mapinduzi ya Sekta ya Maji

Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji vijijini kimeongezeka kutoka asilimia 64.8 mwaka 2019 hadi asilimia 72.3 kufikia mwezi Juni 2021.

Waziri Aweso akiongea jijini Dodoma kuhusu yaliyofanyika katika kipindi cha miaka 60 amesema kuwa hadi sasa, jumla ya vijiji 8,708 kati ya 12,327 vinapata huduma ya majisafi baada ya kukamilika kwa miradi 1,139 ya maji vijijini chini ya utekelezaji wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

Waziri Aweso ameongeza kuwa Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo inatekeleza miradi mbalimbali kupitia programu za malipo kwa matokeo zinazolenga kuhakikisha uendelevu wa miradi ya maji vijijini na jumla ya shilingi bilioni 688.81 zimetumika kuboresha huduma ya maji vijijini.

Aidha, amesema kuwa katika mwaka 2021/22, Serikali imepanga kutekeleza miradi 1,176 ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini dhumuni likiwa ni kufikisha asilimia 85 ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini ifikapo mwaka 2025.

Waziri Aweso amesisitiza kuwa Wizara ya Maji inaendelea na mikakati ya kuboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi kwa kupanga kutumia Shilingi bilioni 139.4 kutekeleza miradi 218 ya maji nchini kote.

Historia inaonyesha kuwa wakati wa ukoloni miradi ya maji ilijengwa kuendana na utashi wa serikali ya kikoloni, hivyo wakati Tanzania Bara inapata uhuru wake hali ya upatikanaji wa huduma ya maji hapa nchini ilikuwa asilimia 25.



*Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akitoa taarifa kwa vyombo vya habari jijini Dodoma kuhusu yaliyofanyika katika sekta ya maji katika miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania bara.*



# "Ushirikishwaji katika kulinda vyanzo vya maji ni muhimu"



Ushirikishwaji wa wadau wote katika jitihada za kusimamia, kutunza na kulinda vyanzo vya maji ili kufikia lengo la kuwa na vyanzo vya maji toshelevu kwa maendelo ya taifa kwa miaka mingi ijayo ni jambo la msingi.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Nadhifa Kemikimba amesema hayo wakati akifungua Jukwaa la Wadau lililojikita katika Kulinda Rasilimali za Maji katika Bonde la Wami-Ruvu kwa dhumuni la kupata suluhisho la kudumu la uhakika wa maji katika chanzo cha Mto Ruvu kwa ajili ya mkoa wa Dar es Salaam na Pwani.

Mhandisi Kemikimba amesema katika Jukwaa hilo lililofanyika jijini Dar es salaam kuwa dhana ya ushirikishwaji kwa wadau wote ni muhimu kwa lengo la kuwa na uelewa na jitihada za pamoja katika kufanikisha uendelevu wa vyanzo vya maji nchini, akitolea mfano umuhimu wa mikakati madhubuti ya kulinda na kutunza Mto Ruvu kwa mustakbali wa mkoa wa Dar es Salaam na vitongoji vyake kuwa na maji ya uhakika ikizingatiwa kuwa ni kitovu cha biashara kwa nchi ya Tanzania.

Amesema lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa maji yanakuwepo ya kutosha kwa matumizi yote, hivyo juhudi za pamoja zinahitajika kutatua changamoto zote zinazotokana na athari za mabadiliko ya tabianchi na shughuli za kibinadamu kwa kukaa pamoja na wadau wote.

Jukwaa limeandaliwa na Wizara ya Maji kupitia Bodi ya Maji ya Bonde la Wami-Ruvu na kwa ufadhili wa UNDP na kuwakutanisha wadau mbalimbali kutoka Wizara ya Maji na taasisi zake, wizara mtambuka, sekta binafsi, AZAKI, na wadau wa maendeleo.



*Wadau wa wanaohusika na rasilimali za maji wakijadiliana wakati wa Jukwaa la Wadau lililofanyika jijini Dar es salaam*





*Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb), pichani akikwea katika tanki, akiwa mkoani Katavi, akifanya ukaguzi wa utekelezaji wa ujenzi unaondelea katika miradi ya majisafi*





Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akishiriki kazi ya kurudisha maji mtoni yaliyochepushwa katika bonde la Wami-Ruvu. Kazi hiyo imefanyika kwa saa 24 katika kuhakikisha huduma ya majisafi inatengamaa katika mikoa ya Dar es salaam na Pwani. Wengine katika picha ni watendaji wa Wizara ya Maji.




# Usikose kufuatilia vipindi vya Maji ni Uhai katika kituo cha Runinga cha Channel Ten.





UHARIBIFU: Vijana wanaochimba mchanga katika eneo la hifadhi ya chanzo cha maji cha Makutupora, Dodoma wakiongea na wataalam wa bonde la Wami-Ruvu ambapo kazi wanayoifanya katika eneo hilo imepigwa marufuku. Makutupora ni chanzo kikubwa cha maji yanayotumiwa na wakazi wa jijini Dodoma. Eneo la hifadhi ya maji la Makutupora lina ukubwa wa kilomita za mraba 2460, ambazo zinakatazo kwa shughuli ya aina yoyote.



*RAHA ya Majisafi: Ni Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb), akijumuika na wananchi, ni baada ya kufungua mradi wa maji wa Kisula, Nkasi mkoani Rukwa*

# Aweso azindua mradi wa kutumia nishati ya umeme jua wa Dola milioni 7.3



*Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb), akiwa na viongozi na wakazi wa Bahi katika kizimba cha huduma ya majisafi kwa malipo kabla, baada ya uzinduzi wa mradi wa kutumia nishati ya umeme jua kusukuma maji.*

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amezindua programu ya kusukuma maji kwa kutumia nishati ya umeme jua katika kijiji cha Zanka, wilaya ya Bahi mkoani Dodoma.
Uzinduzi huo ni matokeo ya utafiti uliofanyika mwaka 2015 uliohusu namna ya kutumia nishati ya jua katika kusukuma maji.

"Teknolojia hii inaenda kupunguza gharama za uendeshaji miradi ya maji ikiwamo ununuzi wa Dizeli" Waziri Aweso amesema katika hafla hiyo iliyohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Wilaya ya Bahi na wakazi wa eneo hilo.

Amesema gharama ya mradi huo ni kiasi cha Dola za Marekani milioni 7.3 na mfumo wa malipo kabla utatumika kwa wananchi kupata huduma ya majisafi.

Waziri ameainisha kuwa mradi huo unatekelezwa katika mikoa mitano ya Singida, Dodoma, Mtwara, Shinyanga na Tabora.

Mradi utanufaisha idadi ya jumuiya za maji vijijini 125 ambazo zinahudumia vijiji 215, vyenye zaidi ya wakazi 560,000 katika wilaya 25.



*RAHA ya Majisafi: Ni Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb), akijumuika na wananchi, ni baada ya kufungua mradi wa maji wa Kisula, Nkasi mkoani Rukwa*




*Zenda mbio siku zenda, zenda za jana na lelo,*
*Zenda mwanadamu zenda, zenda Mungu kimbililo,*
*Zenda ni Yeye hupenda, zenda pamwe na vililo*
*Zenda mwaka wayoyoma, zenda tuvushe salama.*

*Zenda tuseme Yarabbi, zenda tuvushe salama,*
*Zenda tunaomba Rabbi, zenda twaomba huruma,*
*Zenda tumefanya dhambi, zenda epusha kiama,*
*Zenda mwaka wayoyoma, zenda tuvushe salama.*

*Zenda siku zenda mbio, zenda mwaka wayoyoma,*
*Zenda mwambie mwenzio, zenda mwimbie Karima,*
*Zenda ndiye kimbilio, zenda mwingi wa rehema,*
*Zenda mwaka wayoyoma, zenda tuvushe salama.*

*Zenda kwenye nne beti, zenda naweka kijiti,*
*Zenda ninaomba cheti, zenda kwa dua ya dhati,*
*Zenda nivuke niketi, zenda nikawe thabiti,*
*Zenda mwaka wayoyoma, zenda tuvushe salama.*

*B. B. Ndunguru*



Kitengo cha Mawasiliano

Tovuti: www.maji.go.tz